Tulivyo Sikia

MINISTERE DE LA santé

Tarehe 16 Mwezi Wa Saba 2020
Gazeti ya Internews inchini DRC #29

Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.
Kila juma, tunakusanya na kuchambuwa maioni ya jamii (uvumi yani habari zenyi hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana(umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "**Koma Ebola**"

- soundcloud.com/user-740750674
- Facebook.com/komaebola
- @Ebolakoma
- koma-ebola.info



EBOLA

SWALI

Tulisikia kama benyi balipona kisha kufanya ma examens banabaandikia ma ordonnances kusudi baende uza madawa, hii haiko kutafuta tena kulamusha ugonjwa yenyi ilisha isha?

JIBU

Benyi balipona banatunziwaka bila malipo ku ma cliniques zenyi zinapashwa bashurulikia.
Kama kuko madawa zimoya zenyi zinaisha mu pharmacie ya ku clinique, kuko saa banapanaka ordonnance ku mutu mwenyi alisha pona kusudi aende uzia ile dawa fasi ingine.
Siku yenyi atarudia tena kwa munganga, anapashwa leta facture na ordonnance ya ile dawa yenyi aliuzaka kusudi bamurudishiye makuta zenyi alitumikishaka kwa kuuza ile dawa.
Na kwa hivyo mpango ya kufuatilia batu benyi balipona inashurulikia hata na bagonjwa benyi biko na lazima ya transfert na kupata msaada ya banganga benyi habiko bakawaida (ba spécialistes), kwa sababu nia ni kubafuatilia na kubashurulikia ku matunzo ya mwili na ya kisaikolojia (ki akili) kwa kuepuka ugonjwa isitokeye tena.

CORONAVIRUS

SWALI

Ju ya nini hakuna hatua za lazima zenyi zinakamatika kuhusu ma gereza (prison) ju ya COVID-19, ju tunasikia kama gereza (prison) ya MUNZENZE ya Goma ilisha ambukizwa?

JIBU

Hatua zenyi zilikamatika na kanuni zenyi Serkali ya Congo ilikamata zinahusika na kukinga siyo batu tu benyi biko huru, lakini na bale benyi banafungwa.
Kwa kutimiza hatua za kujikinga kwa kupiganisha COVID-19 zilitozotangazwa tarehe 18 ya mwezi ya tatu ya 2020 na raisi (president), mafunzo ya bakubwa benyi kuhusika na afya na bakubwa ba ma gereza (prisons) ilifanyikaka kwa kufuata na kufuatilia zile hatua ndani ya ma gereza (prisons).
Kuhusu bale batu benyi balisha hakikishwa kama banagonjwa mule mu prison ya Munzenze ya Goma, serkali ya jimbo na bashirika bake balisha anzisha ma kazi kwa kusimamisha maambukizi ya Covid-19 mu prison.
Hatua za mingi za kujikinga zimekamatika kwa kufanya kazi kama zifuatazo: kupima homa kwa kuingilia, kuweka kitabu kwa ku chunguza kuingia na kutoka ya bageni, kunawa mikono na kuvala maske inakuwa kanuni kwa kila mugeni mbele ya kuingia mu prison, na kazalika.
Bagonjwa bote ba Covid-19 benyi balipatikana banapata matunzo mu chumba ya upekee ya prison.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE · CROIX-ROUGE DE LA RDC · TRANSLATORS WITHOUT BORDERS · PAUL G. ALLEN FAMILY FOUNDATION · Internews Local voices. Global change. · INTERNATIONAL FEDERATION

Internews I Email: pbahati@internews.org

Tulivyo Sikia

MINISTERE DE LA santé

Tarehe 16 Mwezi Wa Saba 2020
Gazeti ya Internews inchini DRC #29



Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "**Koma Ebola**"

- soundcloud.com/user-740750674
- Facebook.com/komaebola
- @Ebolakoma
- koma-ebola.info

EBOLA

SWALI

Gisi Ebola imeisha tunaweza anza kula nyama za pori?

JIBU

Ina shauriwa kwa wakati huu wa muripuko ya magonjwa na nyuma ya muripuko ya magonjwa kuachana na uwindaji wa manyama za pori, kuacha kuzigusa ao kuzikula ju hazipatake hata uchunguzi moya ya munganga wa manyama.

Hata kama balikuwa bametangaza mwisho ya muripuko ya magonjwa ya Ebola, manyama zimoya zinaweza ambukiza magonjwa ya kuuwa sawa vile Ebola na kuleta muripuko ya magonjwa ya mupya, kufuatana na gisi zile manyama za pori ziko na ma virusi tafauti zenyi zinaweza kuwa hatari kwa mwanadamu.

Batu baliosoma banaonesha kama nyama zimoya njo fasi sana sana kwenyi virusi ya Ebola inaishi tangu ilipotokea mu mwaka wa 1976 mu Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.

CORONAVIRUS

SWALI

Kwa nini ma kesi za bagonjwa ba virusi ya corona ziko zinaongezeka na japo kuko batu benyi biko banapona? Haiko ju ya kutuogopesha kwa kuendelea kutuuwa?

JIBU

Kuongezeka kwa ma kesi za bagonjwa ba Covid-19 mu fasi fulani inatokana na bitu mingi kama vile: kukataa kama ugonjwa iko, ma safari zenyi hazichunguziwe na za uficho za batu kutoka fasi kwenyi ugonjwa ilisha kuwa kwenda kwenyi haiyakuwa, kutoheshimia kanuni za kujikinga ao za kuzuia, na kukatala ao kugangala kufuatiliwa ki afya, ki matunzo, hatua za kuzuia ugonjwa na bingine.

Kujuwa muzuri hibi bitu njo namna moya ya kusimamisha kuongezeka ya ma kesi za batu benyi banagonjwa na hapana kuona batu benyi balisha pona. Inaomba kupana mwangaza kama wakati tunapiganisha ugonjwa, hakuna mutu mwenyi iko na faida ya kuogopesha mwengine ao kumuuwa.

Kushinda vita ya kupiganisha hii virusi ya kuuwa inaomba kila mutu kuhusika kwa kuimaliza. Njo maana siye bote tunaombwa kuheshimia na kuendelea kufuata hatua zote za kujikinga zenyi bakubwa banatupatia kwa kujikinga na kukinga bengine.

Kila mutu mwenyi anaanza onesha ma halama za ugonjwa sawa vile kichwa kuluma, homa na maumivu ya mwili anapashwa enda kwenyi kituo cha afya kwa kujipimisha.

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupitia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID).
Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.